# UHUSIANO

***Kuimarisha maisha yako ndani Kristo***



## Hongera/Pongezi!

Karibu kwenye jamii ya Mungu. Unapo anza uhusiano huu na Kristo, tungependa kukupa mafundisho na maelezo zaidi yatakayo kukusaidia unapo zidi kumtafuta na kumjua Mungu.

Ulipogeuka kutoka mbali na dhambi zako, na kuweka imani yako kwa Yesu krsito, ulianza maisha mapya kama mkristo. Bibilia imetumia maneno mengi kuelezea maisha haya mapya. Inasema kwamba umeokelewa, kumbolewa, kuzaliwa upya, motto wa Mungu, Rafiki wa Mungu, Kiumbe kipya ndani ya Kristo," na mengine mengi. Kulingana na maandiko umepata kitambulisho mpya ndani Ya Kristo.

Sehemu kubwa ya kukua kwako kama Mkristo ni kuelewa na kukubali kitambulisho chako kipya ndani ya Kristo. Utatambua kwamba Ukristo si wewe kuishi kwa ajili ya Mungu, bali ni Mungu kuishi maisha yake ndani yako. Maisha hii inawezekana kama utaweza kutambua maisha yako ndani ya Kristo na kuenenda kulingana na kanuni zake. Kwa muda wa siku saba zifuatazo, kijitabu hiki kitakusaidia kupata majibu ya maswali yafuatayo:

| | |
|---|---|
| **Siku ya Kwanza:** | **Kitambulisho change Kipya ndani ya Kristo ni Nini?** |
| **Siku ya Pili:** | **Uzima wa Milele ni nini?** |
| **Siku ya Tatu:** | **Lengo kuu la maisha ukristo ni nini?** |
| **Siku ya Nne:** | **Ina maana gani kuwa mwanfunzi wa Kristo?** |
| **Siku ya Tano:** | **Nawezaje soma Bibilia?** |
| **Siku ya Sita:** | **Mbona niende Kanisani?** |
| **Siku ya Saba:** | **Naweza kufanya nini ili nikue kama Mkristo?** |

Warumi 8:29 inasema, "Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."

Mungu anataka kubalisha silica au hulka yako iwe kama ya Kristo. Anataka ukue katika kuelewa kwako na kukua kama mkristo. Kiini chetu ni kukusaidia uwe na msingi bora na katika njia bora.

Na Mungu akubariki unapo tambua maisha yako ndani ya Kristo!

## Jinsi ya kutumia kijitabu hiki

1. Utahitaji Bibilia, kalamu, penseli
2. Soma maelezo kwa makini, na jaza pengo unapoendelea
3. Ikiwezekana, jaribu kukipitia kijitabu hiki baada ya kukua Mkristo. Kama umekuwa Mkristo kwa muda, kitumie kijitabu hiki kama nakala hii kama kumbukumbu ya kukuongoza katika Maisha ndani ya Krsito.
4. Shiriki mafundisho haya na wengine mungu akikupa nafasi.

## SIKU YA KWANZA: Kitambulisho change Kipya ndani ya Kristo ni Nini?

**Kitambulisho chetu kinatueleza.** Kutambulika kwetu kunalingana na kile tunacho kifanya, tunacho kipenda, tulipo toka, ama jinsi tunavyo jiona sisi wenyewe. Angalia jinsi watu wanavyo jitambulisha mara ya kwanza. Habari ya ahsubuhi. Jina langi ni Daktari Simms. Mimi ni daktari wa watoto. "Jambo, mimi ni Allen. Nafundisha darasa la saba somo la historia. "Hamjamboni. Jina langu ni Mike. Mimi ni mlevi ." kitambulisho chetu kina tueleza.

Kabla ya Kristo, kitambulisho chetu ilielezwa na kile tulicho fanya pale awali. Warumi 3:23 inatuambia, "Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Haijalishi kama tumetenda dhambi ndogo ama nyingi, kila mtu ametenda dhambi na kila mtu ametambulika kama mwenye dhambi.

Ulipogeuka mbali na dhambi zako kwa kuweka imani yako kwa Kristo, ulipewa kitambulisho kipya. Hautambuliki na dhambi zako tena; mbali na kristo na utakatifu wake. Paulo alisema, "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu..." (Wagalatia 2:20). Kristo anaishi ndani yako.

William Culberston anaelezea mageuzi yako (Kristo kukuokoa na kukupa kitambulisho chake) kupitia mtazamo wa Warumi 6:6-8. "Ni nani aliye kufa msalabani? Ni Kristo bwana wetu aliye kufa msalabani, lakini ni nani mwingine aliye kufa? Kujua hii kwamba utu wetu wa zamani ulisulubishwa nay eye, ili miili ya dhambi iweze kutupiliwa mbali, ndipo mimi na wewe tusiwe tena chini ya utumwa ya dhambi; kwa maana Yule aliye kufa alituweka huru mabli na dhambi. Kwa hivy kama tumekufa na Kristo, tunaamini tutaishi na yeye milele.

Kama Kristo, maisha yako inapata kitambulisho ndani ya Kristo. Alipo kufa msalabani, ulikufa msalabani (Warumi 6:6-8). Alipofufuka kutoka kwa wafu, ulifufuka nay eye pia kutoka kwa wafu (Wakolosai 2:12). Uko ndani ya Kristo na Kristo ndani yako. Yeye ndiye kitambulisho chako!

Haimaanishi uko kwenye kiwango kimoja na Kristo. Inamaanisha kwamba utu wako wa kale umepita na maisha yako mapya yamo ndani ya Kristo (Wakorintho wa Pili 5:17).

Ramani au Chati ifuatayo inaelezea kitambulisho chako kama vile Mungu anavyoelezea

## Je, wewe ni nani?

**Wewe ni chumvi ya ulimwengu** (Mathayo 5:13)

**Wewe ni taa ya ulimwengu** (Mathayo 5:14)

**Wewe ni motto wa Mungu** (sehemu ya familia yake) (Yohana 8:16)

**Wewe ni sehemu ya mzabibu wa kweli** (Yohana 15:1,5)

**Wewe ni rafiki wa Yesu** (Yohana 15:15)

**Umetuliwa na kuchaguliwa na Kristo kuzaa matunda yake** (Yohana 15:16)

**Wewe ni shahidi wake Kristo** (Matendo ya Mitume 1:8)

**Wewe ni mtumwa wa utakatifu** (Warumi 6:18)

**Wewe ni mtumishi kwa Mungu** (Warumi 6:22)

**Wewe ni motto wa Mungu** (Warumi 8:14-15; Wagalatia 3:26; 4:6)

**Wewe ni mrithi pamoja na Kristo** (Warumi 8:17)

**Wewe ni hekalu la Mungu** (Wakorintho wa kwanza 3:16; 6:19)

**Umeunganishwa pamoja na Kristo kwa roho moja pamoja na yeye** (Wakorintho wa kwanza 6:17)

**Wewe ni sehemu oja pamoja na Mwili wa Kristo** (Wakorintho wa Kwanza 12:27; Waefeso 5:30)

**Wewe ni kiumbe kipya** (Wakorintho wa Pili 5:17)

**Umepatanishwa na Mungu na umtumishi upatanisho** (Wakorintho wa Pili 5:18-19)

**Umtoto wa Mungu na pamoja na Kristo** (wagalatia 3:26-28)

**Umrithi wa Mungu** (Wagalatia 4:6-7)

**Wewe ni mteule** (Waefeso 1:1; Wakorintho wa kwanza 1:2; Wafilipi 1:1; Wakolosai 1:2)

**Wewe ni Mfanyakazi wa Mungu** (Waefeso 2:10)

**Wewe unauraia katika familia ya Mungu** (Waefeso 2:19)

**Wewe ni mfungwa wa Wa kristo** (Waefeso 3:1; 4:1)

**Wewe ni mwenye haki na mtakatifu** (Waefeso 4:24)

**Wewe ni raia wa binguni na umeketi binguni wakati huu** (Wafilipi 3:20; Waefeso 2:6)

**Umefichwa ndani ya Kristo kwa Mungu** (Wakolosai 3:3)

**Wewe ni sura ya uzima wa Kristo** (Wakolosai 3:4)

**Wewe mteule wa Mungu, mtakatifu na mpendwa wa Mungu** (Wakolosai 3:12)

**Umeteuliwa na kupendwa na Mungu** (Wathesalonike wa Kwanza 1:4)

**Wewe ni mwana wa mwanga na wala si wa Gizani** (1 Wathesalonike 5:5)

**Wewe ni ndugu mtakatifu, mshiriki katika wito wa Binguni** (Waibrania 3:1)

**Wewe ni mshiriki katika Kristo** (Waibrania 3:14)

**Wewe ni jiwe lenye uhai** (1 Petero 2:9-10)

**Wewe ni taifa teule, kuhani wa kifalme na taifa takatifu** (1 Petero 2:9-10)

**Wewe ni mgeni na asiye wa ulimwengu huu** (1 Petero 2:11)

**Wewe ni adui wa Shetani** (1 Petero 5:8)

**Wewe ni motto wa Mungu** (1 Yohana 3:1-2)

**Umzaliwa na Ibilisis hawezi kukudhuru** (1 Yohana 5:18)

**Wewe ni mwana kondoo kwenye zizi la Kristo** (Zaburi 23 na 100)

**Sehemu kubwa ya Mkristo ni kuanza kujiona katika mtazomo wa Mungu.**
**Chukua wakati wa Kuzingatia sehemu ambazo zina angazia maisha yake sana.**

## Siku Ya 2: Uzima wa Milele ni nini?

Kama mfuasi wa Yesu Kristo, umepewa zawadi ya bure ya Uzima wa milele (Warumi 6:23). Hii ni Habari Njema. Hata hivyo, Wakristo wengi wamechangnyikiwa kuhusu uzima huu wa milele. Wacha tuangazie maana kamili ya uzima wa milele kama vile Mungu mwenyewe anavyo eleza.

Mara kwa mara Yesu aliongelea uzima wa milele. Alisema…

- Yeyote amwaminiye atapata uzima wa milele (Yohana 3:15)
- "Kwa kuwa mapenzi yake Baba Mungu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; name nitamfufua siku ya wmisho." (Yohana 6:40)
- "kwa maana jinsi hii,Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele."Yohana 3:16)
- "…bali yale maji nikayompa yatakuwa ndani yake chemichemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele." (Yohana 4:14)

Kila mahali alipoenda yesu, aliongelea uzima wa milele. Aliileta katika mafundisho yake, Maombi yake kw Baba, na kuwafunza wanafunzi wake. Kulingana na Maandiko, twaambiwa kwamba wote wanaomuamini Kristo watapata uzima wa milele. Lakini, uzima wa milele ni Nini? Haikuwa hadi Yohana 17 wakati Yesu aliopelezea kwa ndani.

- "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."

Uzima wa milele ni kumjua Mungu. Sababu ya Yesu kuuwacha utukufu wa Binguni na kukuja duniani ni kutuwezesha kumjua Mungu. Wakristo wengi wanadhani kwamba uzima wa milele ni kuenda Binguni baada ya kukufa. Lakini kuenda binguni ni faida moja wapo ya kumjua Mungu; na si zawadi kuu.

Zawadi kuu ya Mungu ni yeye mwenyewe. Tumeumbwa tuwe na uhusiano na Mungu, dhambi ilitutenga na huo ushirikiano na uhusiano, na Yesu alikufa na akafufuka ili alete upatanisho na Mungu. Uzima wa milele ni kumjua Mungu katika hali ya uhusiano.

Kama uzima wa Milele ni kumjua Mungu, tunawezaje kumjua Mungu?

**Moja: Mungu Lazima ajidhihirishe mwenyewe.**

**Pili: Lazima tuamini alicho dhihirisha**

**Tatu: Lazima tuwe na wakati na nafasi ya kukaa na kile Mungu amedhihirisha kwetu.**

Mungu amejidhihirisha kwetu kivipi? Amejidhihirisha kwetu ifuatavyo:

- Uumbaji (Zaburi 19:1-4; Warumi 1:20)
- Dhamiri (Warumi 2:14-15)
- Kristo (Yohana 1:1, 5:18, 8:58; 14:9; Waibrania 1:1-2)
- Maandiko matakatifu ya Bibilia (Yohana 20:31; 2 Timotheo 3:16′ 2 Petero 1:21)

Kwa nini ni muhimu kuamini kile ambacho Mungu ametudhihirishia? Imani ni jambo la kina katika kuamini Injili takatifu. Kama tulivyo jifunza pale awali kwenye kurasa za kwanza, Uzima wa Milele hupewa wale walio amini Kristo. Ina maana kwamba mtu anamuamini Yesu ndiye Mwana wa Mungu na kwamba alikufa msalabani, alifufuka kutoka kwa wafu, na anapeana uzima wa milele. Msingi ya Injili ni Kristo na kazi aliyo ifanya Msalabani.

Kumalizia, ni lazima tuwe na wakati wa kushiriki na aliye jitambulisha kwetu. Njia ya pekee ya kumjua mtu ni kushiriki pamoja na huyo mtu. Unaweza jifunza kuhusu fulani kwa kusoma kitabu, lakini utamjua huyo mtu kwa kushiriki naye na kuwa na wakati wa kukaa naye. Unapokuwa na mtu, utaanza kufahamu tabia yake, anacho kipenda na kuchukia, hisia zake, maoni yake kuhusu mambo tofauti, moyo wake, anavyo fikiria, na anavyo fanya mambo yake. Unaweza kumjua mtu punde tu unapo anza kushiriki naye na kuwa na wakati naye.

Wacha tuweke vipengele hivi pamoja. Karama ya Mungu ni Uzima wa milele. Uzima wa milele ni kumjua Mungu. Tunamjua Mungu kwa sababu amejidhihirisha mwenyewe kwetu, na kwa kuamini alicho kidhihirisha kwetu, na kuwa na wakati wa kushiriki pamoja naye.

Angalia kwenye Bibilia yako Yohana 15:1-8. Ni mara ngapi Kristo ametuamuru kukaa ndani yake? Kukaa ina maana kwamba kuketi naye, kubaki ndani yake, kuwa naye nyumbani. Kulingana na maandiko uliyo soma, kukaa ndani ya Kristo kuna kusaidiaje kumjua Mungu?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Mungu amejidhirisha kupitia Maandiko. Sehemu moja ya kumjua Mungu ni kuamini kile alicho kidhihirisha kwetu. Angalia Wakolosai 1:15-19. Ni nini ambacho Mungu amekidhirisha kuhusu yeye mwenyewe? Andika chini sifa tano muhimu ailiyo tajwa. Je! Waiamini?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## Siku ya 3: Ni nini Lengo la Maisha ya Ukristo?

Kama karama ya Mungu kwetu wanadamu ni Uzima wa milele (kumjua Mungu), kwa hivyo lengo letu kuu lazima iwe ni kuipokea karama hii. Kwa hali nyingine, sehemu hii ya tatu ni maendelezo ya mafundisho ya jana. Sasa kwa vile tuna ufahamu wa dhabiti wa kina cha Uzima wa milele, tunaweza fahamu lengo kuu la maisha ya Ukristo.

Lengo la maisha ya Mkristo ni nini? Lengo hili lina sura mbili:

### LENGO KUU NI KUMJUA MUNGU

Tunaipokea karama ya Uzima wa milele kwa kumjua Mungu. Inaturudisha nyuma katika kusudi la uumbaji. Tuliumbwa tuwe na ushirika na Mungu. Nayo inaturudisha katika lengo la pili. Unawezaje kumjua mtu kwa ukweli?

### LENGO NI KUSHIRIKI NA KUWA NA WAKATI NA MUNGU

Tulipo ona jana, jinsi ya ya kumjua mtu ni kuwa na wakati naye katika ushirika. Unaweza kumfahamu mtu kupitia hali ya kusoma kitabu, lakini unaweza kumjua ukiwa na wakati naye na ukishiriki naye. Wacha tuangalie kwa undani jambo hili.

Hebu fikiria hali ya kuchumbiana. Kiini cha kuchumbiana na mwingine ni kumjua kwa undani ili uangalie kama unaweza kuishi naye. Munapo chumbiana utaenda anapo enda; utafanya atakacho fanya; utajaribu kuelewa moyo wake, mienendo yake na tabia na hata mipango zake. Kwa kuwa na wakati naye na kushiriki pamoja, husaidia kumfahamu hali na mienendo yake, hisia zake na mawazo yake. Baada ya muda fulani utamjua kwa kina na vina.

Katika hali hio, ndivyo tunapaswa kumjua Mungu. Unawezaje kuwa na wakati na Mungu? Kuna jinsi kadha umepewa. Nyingi za hizi mwongozo zina fahamika kama " taratibu" ya Imani ya Mkristo.

- **Kusoma Bibilia ni njia moja ya kushiriki pamoja na Mungu na kumjua.** Bibilia ni ufunua wa Mungu wake kwetu. Mungu ametuthihirishia sifa na silica yake kwetu, moyo wake, matarajio yake kwetu, na mipango yake. Unaposoma Bibilia zaidi ndivyo utakavyo mjua na mfahamu Mungu.

- **Kuongea na Mungu kwa maombi ni njia moja ya kuwa na wakati naye na kumjua zaidi.** Maombi si kumuambia Mungu kila unacho taka; maombi ni pia ni kumsikiliza Mungu anapo nena na wewe. Huchukua muda kufahamu na kupambanua sauti ya Mungu katika maombi. Hata hivyo, unapo kaa pamoja na Mungu, ndivyo utamtambua Mungu na sauti yake.

- **Kuabudu Mungu ni njia moja ya kuwa na wakati na Mungu na kumjua zaidi.** Kuabudu si kuimba pekee. Tunamuabudu Mungu na maisha yetu, uamumuzi wetu, matendo yet, mienendo yet ya maisha. Kuabudu kunaweza kuwa dhahiri isiokuwa na mambo mengi, bali ni katika hali ya kumshukuru Mungu way ale ametenda, na kutii sheria zake na maagzo yake.

- **Kusikiliza mafundisho ya Bibilia na mahubiri ni njia moja ya kuwa na ushirika na Mungu na Kumjua.** 2 Timotheo 2:15 inasema, "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli." Hakuna anaye weza kumjua Mungu kwa uwezo wao. Ukristo unahitaji ushirika pamoja na Wakristo wengine. Unaposikiliza mafundisho ya bibilia na mahubiri, inakuelekeza kwa Kristo, inamuinua Kristo, inakuhimiza katika imani ndani ya Kristo, kushiriki katika mafundisho ya Kristo, n.k.. Hivi vyote vitakusaidia kumjua Mungu zaidi.

- **Kuwa na wakati na Maumbile ya Mungu ni njia moja ya kushiriki pamoja na Mungu na kumjua zaidi.** Warumi 1 inatuambia kwamba hali ya Mungu inadhihirishwa kupitia maumbile yake, uwezo wake, mienendo yake na nguvu zake pia. Muandihsi wa Zaburi ametuhakikishia kwamba mbingu imejaa na utukufu wake. Wakati ufunuo wa ndani umedhirishwa kupitia Bibilia, ufunua mwingine ni wajuu kupitia Muambile yake.

**Haijalishi njia au hali utakayo chagua,<br>lengo kuu ni kushiriki pamoja na Mungu na kumtazamia yeye pekee.**

Wacha turejelee haya maudhui. Lengo kuu ni kumjua Mungu. Walakini si kumjua Mungu tuu pekee, bali ni kuifahamu Biblia kwa undani. Lengo ni kumfahamu Yeye. Ni kweli mtu anaweza tumia muda wake wotemaishani kujifunza juu ya Mungu, kufanya vitu vya kiroho, lakini hakose kumfahamu.

Lengo la kila siku ni kuwa na wakati na Mungu. Tunahitajika kuwa na mikakati kabambe ya kutuleta karibu na Mungu ili tumfahamu zaidi. Lengo la kwanza lina tufahamisha maishani na la pili kuhusu maisha ya kila siku. Kama Mkristo atatilia maanani haya mambo mawili na kuyapa kifua umuhimu wa kwanza hata akilini, yata muezesha kuwa na ufahamu mwafaka na kuishi kama mfuasi halisi wa Kristo.

Kulingana na vile tunavyo paswa kuwa na wakati na Mungu (kutokana na mafundisho ya awali), taja vitu kadhaa unvyo weza anza leo kufanya.

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

Kama lengo ni kunfahamu Mungu wa Bibilia, ni nani anaye weza kukusaidia kufikia lengo hili? Taja watu and aina ya watu wanao weza kukusaidia. Uwafikie wengine ulio wataja hapa.

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

__________________________________________________________

## Siku ya 4. Ina maanisha nini kuwa mwanfunzi wa Kristo?

*"yesu akaja kwao, akasema nao akawaamba, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Mathayo 28:18–20)

Kuna maswali mawili ya kuongelewa hapa kutoka kwenye kifingu hiki cha Bibilia. Nini maana ya Mwanafunzi? Wanafunzi hutoka wapi?

Katika ilivyo tambulika na Wayahudi wa karne ya kwanza, mwanafunzi ni Yule aliye tumia muda wake mwingi na mwalimu wake rabi (akimsikiliza, kumtizama, na kumuiga) ili waweze kuwa kama mwalimu wao na wawe wanweza kufundisha wengine yale walio pokea kutoka kwake.

Katika Agno jipya, Yesu anaitwa "Mwalimu" mara kumi na tatu. Yeye ni mwalimu wetu nasi tu wanafunzi wake. Kama wanafunzi, tunapaswa tuwe na wakati wa kukaa na mwalimu wetu (tukimsikiza, kumtizama, na kumuiga) ili tuwe kama yeye, na mwishowe tuwafunze wengine tuliyo pata kutoka kwake.

Unapo kuwa na wakati na Kristo, atakuelekeza katika sehemu nne muhimu. Atakuelekeza katika kumpenda, kuungana na waumini wengine, kuihudumia ulimwengu, na kuwapa wengine Injili. Maisha yote ya Mkristo in ishara hizi zote nne katika Kufuata Kristo kikamilifu.

**Kumpenda Mungu ni...**

- Kufurahia uhusiano wa karibu na Mungu
- Kupata kumfahamu Yeye kupitia neno lake
- Kuwasiliana na Mungu kupitia Maombi
- Kushiriki pamoja naye
- Kumuabudu kwa njia ya maisha yetu
- Kuishi kulingana na amri ya kwanza na kuu (Mathayo 22:37–38)

**Kuungana na waumini wengine...**

- Kufurahia na kujenga uhusiano wa karibu na wakristo wengine
- Kuungana katika huduma, maombi, utumishi, maono, upendo, na mafundisho ya Bibilia, n.k.
- Kutambua kwamba ukristo unapatikana katika ushirika pamoja na wengine
- Kupenda na kuhudumia wakristo wengine

**Kuhudumia ulimwengu ni...**

- Kuwaonyesha watu upendo kupitia matendo yetu – si kwa maneneo yetu pekee
- Watumishi wazuri wa ulimwengu na raslimali yake
- Kufuata mfano wa Kristo kuwahudumia wengine
- Kupeana maisha yetu katika maisha yaw engine, katika jamii, na Taifa kwa jumla


**Kukabidhi Injili ni...**

- Kushiriki Injili ya ufalme
- Kukabidhi mafundisho ya Kristo kwa wengine
- Kuwaalika wengine waje kushiriki katika kazi ya Ufalme wa Mungu

Ukiyaondoa majengo ya makanisa, taarifa ya gharama, ratiba ya ibada, kuwa mwanafunzi inahusu Kumfuata Kristo. Tunapo mfuata Kristo, anatuongoza katika upendo, anatuleta karibu na Wakristo wengine, katika kuhudumia ulimwengu, na kukabidhi injili kwa wengine.

Safari ya kila mmoja na Mungu itakuwa tofauti, lakini kama majukumu ya wanafunzi itabaki kuwa sawa. Kristo atatuelekeza katika upendo, umoja, huduma, na kushiriki katika neno.

Kwa vile umeona jinsi ya mpangilio huu, inaweza kutuongoza kama dira ya kiroho. Ukitaka kuhakikisha njia yako ya maisha inaenenda katika kukomaa ndani ya Kristo, iweke kweli hizi maishani mwako na umuulize Mungu akujulishe ulipo pungukiwa. Kumpenda Mungu lazima iwe kaskazini ya hali yako ya kiroho. Sehemu zile zingine katika dira yako ya kiroho huenenda vizuri ikiwa tutazingatia kumpenda Mungu kwanza.




Unapo weka dira hii ya kiroho maishani mwako, unaweza ona sema ya maisha yako unayo paswa kurekebisha. Unaweza pata kwamba hauna wakati wa kushiriki pamoja na Mungu. Pengine hauna ushirika na wengine, hauwaelezi neno na huduma yako kwa wengine imedidimia. Unapo tambua ukosefu wako katika yeyote, muombe Mungu akufunulia na umpe nafasi aishi ndani yako na kukuelekeza katika ukosefu wako.

Kutokana sehem nne tulizo zi taja, ni sehemu gani maishani mwako unao huo ukosefu? Ni nani unaye weza ongea naye ili umuhusishe?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Tumeitwa kuwa wanafunzi na kuwafanya wengine wawe wanafunzi. Ni nani unaweza kujifunza kwake (Taja majina yao) na ni nani unayeweza shiriki naye (taja majina yao)?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## Siku ya 5. Nawezaje kujifunza Bibilia?

Maelezo yafuatayo yana patikana ndani ukurasa wa kwanza wa Bibilia ya Gidioni. Aliye nukuu maandishi haya hajulikani, lakini maandiko yenyewe ni mwafaka. Kitabu kinacho ongelewa ni Bibilia.

> "kitabu hiki kina mawazo ya Mungu, hali ya mwanadamu, njia ya wokovu,maangamizo ya wenye dhambi na furaha ya aliyeokolewa. Mafundisho ya kidini ni matakatifu, maagizo yake ni ya kweli na kuaminika, historia yak e ni ya kweli, na maamuzi yaki hayawezi badilika au kupingwa. Uisome uwe na hekima, iamini uwe salama na utende maagizo yake uwe mtakatifu.
>
> Iko na mwangaza ya kunionyesha njia, chakula ya kunitosheleza, kunituliza ya kunipa furaha. Ni ramana ya msafiri, ni bakora ya mhaji, dira ya rubani wa ndege, silaha ya mwanjeshi, na ni tabia ya Mkristo.
>
> Hapa tunapata paradise tena, mbingu zinafunguliwa na malango ya kuzimuni zina fungwa. Kristo ndiye msingi na anaye ongelewa hapa, mazuri yangu inafichuliwa na utukufu wa Mungu ndio kina na vina. Inapaswa kuijaza fikira zetu, kutawala mioyo na kuongoza miguu yetu.
>
> Isome kwa utaratibu, kila mara na kwa hali ya Maombi.
>
> Nimepewa mimi maishani, itafunguliwa siku ya hukumu na itakumbukwa milele. Ina jukumu ya hali ya juu, itamlipa mfanyikazi muaminifu na ita muhukumu anaye shusha na kudunisha mafundisho yake.

Maelezo haya kuhusu Bibilia ni ya uzito sana nay a kweli. Walakini, tunataka kukupa fafanuzi ya rahisi kuhusu Bibilia.

**Bibilia ni ufunuo wa Mungu wake mwenyewe kwetu wanadamu.**

Kujifunza Bibilia ni ya muhimu kwa kwetu kama wanafunzi. Mafundisho yote ya dini na imani na shawishi zote ni lazima zichunguzwe kutumia Bibilia. Maswali yafuatayo yamejibiwa kupitia kujifunza Bibilia.

- Nawezaje kujua ukweli?
- Nawezaje kujua yale Mungu anahitaji kwangu?
- Nawezaje kumjua Mungu?
- Nawezaje kujua imani yangu ndio ya kweli?
- Nawezake kujua kuongoza Jamii yangu?
- Nawezaje kujua kutembea na kuishi kama mwanfunzi?

Maswali kama haya yote yata jibiwa unapo jifunza na kusoma Bibilia. Timotheo wa pili 3: 15–17 ina sema, "*...nay a kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

## Kuna mawazo kadhaa ya msingi ya kuweka maanani tunapo jifunza Bibilia.

**1. Maandiko matakatifu ni Neno la Mungu.**
- Maandiko ni pumzi ya Mungu (2 Timotheo 3:16a)
- Ni pumzi ya Mungu katika mafundisho, haina mawaa wala makosa ilipoandikwa kwa mara ya kwanza, mafundisho yenye hakika isiyo na kosea.

**2.Roho Mtakatifu ndiye anayetuwezesha kuelewa**

*"lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hata nena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake." (Yohana 16:13)*

Kama Mkristo, Roho Mtakatifu hayuku tu na wewe bali yuko ndani yako (Yohana 14:17).

**3. Maandiko yana tafsiri Maandiko**
- *"...Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."*

*Kama hauelewi kifungu cha maandiko, iruhusu Maandiko ijibu swali lako yenyewe.*

**4. Mazingira hufungua maana**

Ndipo uelewe kufungu cha maandiko, ni lazima utambue yafuatayo:

- **iMuandishi:** Ni nani aliye andiko kitabu hicho
- **Wasomaji:** ni akina nani walioandikiwa kitabu hicho
- **Matukio wa wakati huo:** ni nini kilicho kua kikifanyika kwa walioandikiwa na muandishi
- **Kusudi/sababu:** kwa nini kitabu kiliandikwa
- **Jinsi ya uandishi/tanzu:** muandishi alitumia aina gani ya uandishi wake wa kitabu

*Maelezo haya unaweza kupata kayika kurasa za kwanza za kila kitabu*

**5. Kuna tafsiri moja ya maandiko lakini matunizi yake ndio tofauti**

Tafsiri ni omoja na dhahiri katika hali yake ya awali. Tukijua tafsiri ya kwanza na maana yake na kusudi ya kuandikwa kwake na walioandikiwa, tunaweza tumia kweli ya neno hilo kwa maisha yetu.

**6. Lengo kubwa ni kumjua Yeye**

Lengo kuu ya kusoma Bibilia si ya kuwa na maarifa pekee; bali ni kumjua na kumfahamu Mungu. Kusoma Bibilia huchukua muda na uthabiti kamili bila kigeugeu. Hauwezi kuelewa kila kitu mara ya kwanza. Ziandike maswali chini, muombe Mungu akupe ufahamu, na umpe wakati wa kujibu maombi yako.

Anza kusoma bibilia yako Leo. Ikiwa haujui pakuanzia, anza na kitabu cha Injili kulingana na Yohana.

## Siku ya 6. Mbona ni hudhurie kanisa?

Pengine umewahi kumsikia mtu akisema, "Nampenda Mungu, lakini si lazima niende kanisa kuthibitisha hiyo." Wako sawa kusema hivyo. Yesu hajatuambia, "Na hivi ndivyo tutajua kwamba munanipenda-ikiwa mutaudhuria kanisa kila jumapili."

Kama kuenda kanisa haitajiki ili kuonyesha jinsi tunavyompenda Mungu, ni kwa nini tuende Kanisa?

Jibu lake laweza kukushangaza. Sehemu ya kukua kwako ndani ya Kristo inafanyika tu ukiwa kati ya waumini wengine kwa ushirika. Ni kama kujaribu kuwa mwana soka hodari ukiwa peke yako. Kuna mambo mengi unaweza jua ukiwa peke yako; lakini baada ya muda unahitaji wengine kufahamu ujuzi zaidi kuhusu mchezo wako.

Ukristo ni mchezo unaohitaji kikundi cha wachezaji. Ni kweli twaweza jua kweli tukiwa peke yetu; lakini kweli hizi zitapata maana na manufaa katika kikundi na katika ushirika na wakristo wengine. Ukitaka kufikia lengo lako kwa nini Mungu alikuumba, itafanyika katika jamii kubwa ya wafuatao maandiko ya Bibilia.

Kuabudu kila Juma kunachangia kukua kwetu kiroho na maisha kama ifuatavyo:

**1. Ni pahali pa kukutana na wakristo wengine.**
Soma Matendo ya Mitume 2:44-46

**2. ni pahali pa kumuabudu Mungu kama jamii ya Kristo.**
"Haleluya. Mshukuruni Bwana, liitieni jina lake, Wajulisheni watu matendo yake" (Zaburi 105:1)

**3. Ni pahali pa kusiliza maandiko yakifundishwa.**
"wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate , na katika kusali." (Matendo ya Mitume 2:42)

**4. Ni pahali pa kuwa hudumia watu wengine.**
"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu." (1 Petero 4:10)

**5. Ni pahali pa kupata himizo na mawaidha ya kibibilia.**
"...wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia." (Waebrania 10:25).

**6. Ni pahali pa kupata changamoto.**
"Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake." (Mithali 27:17)

Katika Waefeso 4, Paulo anatufunza jinsi kila mmoja katika mwili wa Kristo ni wa maana na ana umuhimu wake na tena anahitajika. "...kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo." (Waefeso 4:16b) Kila Mkristo anakitu cha kuongezea kanisani. Tukiwa tayari kutumika, na kuwahudumia wengine na kwa pamoja – mwili mzima utakua vizuri na kwa upendo.

Akiongea na kanisa la Korintho, Paulo anawaambia kwamba kama kanisa wanategemeana. "… ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe." (1 Wakorintho 12:25). Si tu kwamba inapendeza kuwa na Wakristo wengine bali ni Muhimu. Twahitaji kila mmoja. Sehu ya kukua kwetu ndani ya Kristo inafanyika katika ushirika na wakristo wengine.

**Unawezaje kupata kanisa/kikundi cha wakristo wengine wanao weza kukusaidia kukua?**

- Omba Mungu akupe utambuzi na muongozo
- Tafuta kanisa ambalo linafundisha neno la Mungu kwa uaminifu
- Angalia kanisa ambalo lina sisitiza mafundisho ya kukuza watu kuwa wanafunzi wa Kristo na kukua ndani ya neno kwa upendo, ushirika, huduma na kuwafunza wengine na Neno
- Waulize maswali kuhusu maono yao, wito, imani, huduma, uongozi, n.k.
- Jaribu kuhusika nao
- Ikiwezekana jiunge nao, la sivyo tafuta kanisa linguine.

Je, unalo kanisa unalohudhuria? Linafikia maelezo tuliokupa? Kama sivyo ni nini linakosea?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Kama hauna kanisa unalohudhuria, andika chini makanisa ambazo ungependa kuenda katika uchunguzaji. Andika majina ya wakristo unao wajua wanao weza kukusaidia kufanya utafiti ukitafuta.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

## Siku ya 7. Naweza fanya nini ili nikue kama Mkristo?

Kuna vitu kadhaa ambavyo vina weza kukusaidia kukua kama Mkristo. Ni muhimu uvielewe na kwa nini tuvifanye.

**ikiwa tutafanya vitu hivi bila kujua umuhimu wake na sababu, basi vitatuelekeza kwa dini wala si ushirika na uhusiano.**

Majukumu yangu kwanza ni nini?

**1. unapaswa kubatizwa.**

**Ubatizo** ni tendo la kujitambulisha na kutii amri ya Kristo. Katika ubatizo, twajitambulisha na maisha ya Kristo, kifo, kuzikwa na kufufuka kwake (Mathayo 3:13-17). Tunapo batizwa, tunatii mafundisho ya Kristo katika agizo lake kuu (Mathayo 28:18-20; Mariko 16:16; Matendo ya Mitume 2:38)

Ubatizo wa Bibilia unafanyika baada ya wokovu ni ya kuingia ndani ya maji. Kubatizwa haumuokoi yeyote bali ni kujitambulisha mbele ya kanisa na watu kuwa umemuamini Kristo na we ni mmoja na wale wengine walioamini.

**2. kuwa na wakati pamoja na Mungu kila siku.**

tuliangazia umuhimu wa maombi pale awali kama njia moja ya kuwa na wakati na Mungu siku ya 2, 3, na 4. Lengo kuu ya maisha ni kumjua Mungu; na lenge la kila siku ni kuwa na wakati na Mungu. Kuna njia nyingi ya kuwa na wakati na Mungu. Lakini, njia bili kuu ni kwa njia ya maombi na kusoma Bibilia.

**a. Maombi**

Maombi ni kushiriki na Mungu kumueleza yaliyomo moyoni mwako, na kusikiliza Mungu anapo nena na wewe yaliyomo moyoni mwake. Chukua maombi kama mazungumzo kati ya marafiki wawili. Ikiwa mmoja ndiye atakuwa akiongea-itakua ni mazungumzo ya binafsi. Watu wawili wakiongea pamoja ni Mazungumzo.

Huchukua muda ili mtu apate kuwa na masikio ya kusikia sauti ya Mungu. Sauti ya Mungu katika maombo haiwezi kukanusha sauti ya Mungu katika maandiko. Mungu atajibu maombi kila mara unapomuomba, unapomuuliza jambo, na unapo nukuu maandiko. Maombi na Bibilia huambatana.

**b. Soma na kuweka akilini maandiko**

Tayari tumeguzui jinsi ya kusoma Bibilia, lakini mbona tusome Bibilia? Twasoma Bibilia ili tumjue Mungu, moyo wa Mungu, mwongozo wake, njia zake, n. k. Bibilia lii hai (Waibrania 4:12). Bibilia ni Neno la Mungu, nay eye huitumia kunena na watu wake.

Utaanzaje kusoma Bibilia? Hapa pana mapendekezo ya kukusaidia:

- Soma Injili ya Yohana (kifungu kila siku). Uliza maswali mawili. Yesu ni Nani? Inamaanisha nini kuwa Mfuasi wa Yesu? Andika chini majibu na ukinakili mstari wa Bibilia.
- Soma kitabu cha Mithali (kifungu kimoja kila siku kwa siku 31)
- Soma Agano Jipya (Mathayo –Ufunuo). Ukisoma vifungu tatu kila siku itakuchukua miezi mitatu kumaliza kusoma Agano Jipya.
- Soma Bibilia nzima (Mwanzo –Ufunuo). Kuna njia tofauti ya kusoma Bibilia kwa mwaka moja. Unaweza kupata kutoka kwenye mtandao au ununue Bibilia unayoweza kuisoma kulingana na mpangilio wa mwaka moja na kukuelekeza kwenye vifungu vya Maandiko kutoka Agano la kale hadi Agano Jipya kila siku.

Unapopata mistari ya Bibilia ya msingi wa tuni, jaribu kuweka kwenye kumbukumbu. Mungu atakukumbusha hayo maandiko unapo muendea kwa maombi.

**3. Jiunge na Kanisa lililoko karibu na wewe.**

Tumeongela umuhimu wa kuwa katika ushirika wa kanisa lililoko karibu na wewe katika siku ya 6. Ili ukue kama Mfuasi wa Yesu Kristo, unahitajika uwe na ushirika na Wakristo wengine. Hizi ndizo mojawapo wa za njia ya kukua:

**a. Kushiriki katika Kuabudu**

Kushiriki katika kuabudu ni njia moja ya kumpa mungu ibada yetu na kuonyesha upendo wetu kwake. Tunatambua Yeye ni nani na kile ametutendea kupitia Maandiko. Twamuambia upendo wetu kwa sauti, kupitia maombi, kuimba, mafundisho na katika mazungumzo.

**b. Jiunge na kikundi kidogo cha chuo cha Jumapili cha Bibilia**

Vikundi vidogo husaidia katika kujijenga na kua na urafiki na nafasi ya kuuliza maswali. Makundi madogo huharakisha kukua kwa mtu ndani ya Kristo.

**c. Mtolee Mungu kwa Kazi yake**

Kutoa ni hali moja ya kumuabudu Mungu na tumaini. Bibilia inatuambia kwamba Mungu ndiye anamiliki kila kitu, na ametukabidhi sehemu ya mali yake. Ametuamuru kumpa asilimia 10 ya zaka zetu. Mkristo anapo toa zaka kwa Mungu, ni njia moja ya kumtii Mungu na kumpa tumaini letu kwake. Wanatii amri ya Mungu, kutumaini Mungu kwa yote a asilimia 90% bali si asilimia 100%.

**d. Jiusishe katika Huduma**

Ungea na Mchungaji, tafuta na utambue vipawa vyako vya kiroho, upate mahali unaweza kuwa wa msaada katika kanisa na fahamiana na watu wengine.—Jihusishe. Wakristo wanapo jipa kwa hiari yao kutumika wanapata nafasi ya kuungana na wengine. Ukingoja uitwe au kualikwa, utangoja sana. Chukua hatua ya kwanza.

Katika haya yote, kumbuka lengo letu kuu. Lengo letu si kutimiza majukumu ya dini; lakini lengo ni Kumjua Mungu. Wacha kusoma kwako Bibilia, Maombi, na kuhusika kwako kanisani ikulete karibu na Mungu.

Muhtasari ya Kuongezea:

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## HITIMISHO

Katika siku 7 zilizo pita, tumepitia na kuangalia nguzo kadhaa za maisha ya Mkristo aliye okoka majuzi. Haimaanishi kwamba tumeongelea maisha yote ya Mkristo. Hatujaanza mafundisho ya thiologia hata kidogo, Kushi kikristo, sehemu yetu na urithi wetu ndani ya Kristo, n.k. Hata hivyo, tumeguzia:

- kitabulisho chako ndani ya Kristo
- uzima wa Milele
- Lengo au malengo ya maisha ya Mkristo
- maana ya kuwa Mwanafunzi wa Kristo
- Jinsi ya kusoma Bibilia
- Umuhimu wa kuwa kwa Kanisa lililoko karibu na wewe
- hatua za kukua ndani ya Kristo

**Mafundisho haya yamefunzwa kwa wiki moja, lakini yanapaswa kufuatiliwa na kutendwa katika maisha yote ya Mkristo.**

Unapo soma zaidi Maandiko, endelea katika ibada na wakristo wengine, ushiirika—ndipo Mungu atakusaidia kujaza mapengo yaliyo baki kwa undani maishani mwako.

Ukumbuke kwamba Ukristo si mbio za masafa fupi bali ni mbio za masafa marefu(marathoni). Jifunze misingi ya ukristo vizuri, na utakua na kukomaa baada muda mrefu. Unapoendelea ndipo utatambua umuhimu wa kujua na kufuata ukweli:

**Kila Kitu Mungu angependa kufanya ndani na kupitia maisha yako, atatimiza kupitia kububujika kutokana na uhusiano wako na Kristo. Kila kitu wala si vitu kadhaa—KILA Kitu.**